**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA**

**16 MEI, 2017**

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA SITA TAREHE 16 MEI, 2017

## I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mwenyekiti) alisoma Dua na kuongoza Bunge.

**Makatibu mezani:**

1. Ndugu Theonest Ruhilabake
2. Ndugu Asia Minja
3. Ndugu Joshua Chamwela

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

(i) Mhe. Charles John Mwijage aliwasilisha Mezani Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(ii) Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliwasilisha Mezani Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(iii) Mhe. Jumanne Kidera Kishimba aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

(iv) Mhe. Masoud Abdallah Salim aliwasilisha Mezani Taarifa ya Kambi ya Upinzani kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## III. MASWALI

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 209: Mhe. Dkt. Pudenciana Kikwembe

Nyongeza: Mhe. Dkt. Pudenciana Kikwembe
Mhe. Pauline Gekul
Mhe. David Cosato Chumi

Swali Na. 210: Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye

Nyongeza: Mhe. Eng. Atashasta Justus Nditiye
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke
Mhe. Almas Athuman Maige
Mhe. Cecilia Daniel Paresso
Mhe. Savelina Silvanus Mwijage

### WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 211: Mhe. Daniel Edward Mtuka

Nyongeza: Mhe. Daniel Edward Mtuka
Mhe. Daimu Iddy Mpakate

Swali Na. 212: Mhe. Mussa Bakari Mbarouk

Nyongeza: Mhe. Mussa Bakari Mbarouk
Mhe. Saumu Heri Sakala
Mhe. Moshi Selemani Kakoso

Swali Na. 213: Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (liliulizwa na Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni)

Nyongeza: Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni
Mhe. Martha Moses Mlata
Mhe. Pascal Yohana Haonga
Mhe. Joseph Roman Selasini

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI

Swali Na. 214: Mhe. Frank George Mwakajoka

Nyongeza: Mhe. Frank George Mwakajoka
Mhe. Mohamed Chuachua
Mhe. James Francis Mbatia
Mhe. Halima Abdallah Bulembo
Mhe. Esther Nicholas Matiko

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Swali Na. 215: Mhe. Esther Michael Mmasi

Nyongeza: Mhe. Esther Michael Mmasi
Mhe. Shaban Omary Shekilindi
Mhe. Khadija Nassir

Swali Na. 216: Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King

Nyongeza: Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King

Swali Na. 217: Mhe. Susan Peter Masele (liliulizwa na Mhe. Suzana Mgonokulima)

Nyongeza: Mhe. Suzana Mgonokulima
Mhe. Rhoda Kunchela
Mhe. Maryam Salum Msabaha

## WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 206: Mhe. Esther Lukago Midimu

Nyongeza: Mhe. Esther Lukago Midimu
Mhe. Augustina Lukago Midimu

## IV. MATANGAZO

- Wageni mbalimbali walitambulishwa Bungeni wakiwemo Viongozi wa Jeshi la Wananchi Tanzania.

## V. MIONGOZO

1. Mhe. Pascal Yohana Haonga – aliomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na 101 (4) kuhusiana na nafasi za kuchangia wakati wa Mshahara wa Waziri kuzingatia uwiano. Je, ni sahihi kiti kuchukua Wabunge wa Upande mmoja tu.

   Kiti kilitoa uamuzi kuwa Mbunge atumie Kanuni ya 5 (4) kuwasilisha Malalamiko yake dhidi ya Kiti.

2. Mhe. Hamidu Hassan Bobali - alitumia Kanuni ya 68(7) na 69 kuomba mwongozo juu ya Uvamizi wa Tembo uliofanyika Jimboni Nkinga ambapo mazao na Nyumba za Wananchi zimevamiwa.

   Kiti kilitoa uamuzi kuwa Mbunge akae na Serikali (Waziri) ili wajadili suala hilo.

3. Mhe. Kasuku Samson Bilago - alitumia Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuhusiana na kitendo cha Askari Polisi kutumia silaha dhidi ya Ndg. Adam Malima kutokana na kosa la kupaki vibaya.

   Kiti kilitoa maelekezo kuwa Bunge halina Taarifa hizo na suala hilo halijatokea Bungeni mapema.

## VI. HOJA ZA SERIKALI

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi alisoma Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake kwa Mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Adadi Rajab – Mwenyekikit wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama aliwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kabla ya Msemaji wa Upinzani kusoma taarifa yake, kiti kilitoa taarifa kwamba Spika ameagiza Aya ya 3 ukurasa wa 2 na Aya ya 3 ukurasa wa 10 ziondolewe kwani zimekiuka Kanuni ya 64 (1) na kuagiza Msemaji wa Upinzani kutozisoma aya hizi. Baada ya taarifa hiyo ya Spika, Mhe. Mwita Waitara alisoma taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

## Mwongozo wa Spika

Mhe. George Mkuchika aliomba Mwongozo kama Bunge linaruhusiwa kuhoji amri iliyotolewa na Kamanda Kuhusu kuongeza muda wa kazi.

Mhe. Cecilia Paresso – aliomba mwongozo kwamba kwa nini Msemaji wa Upinzani asimalize kuisoma kama ilivyo utaratibu na hasa ikizingatiwa Spika ametoa maelekezo ya maeneo ya kuondolewa.

Kiti kilitoa mwongozo kwamba Mbunge yeyote anaweza kuomba Mwongozo na kuagiza maneno yanayohusu muda wa kazi kuongezwa Jeshini yaondolewe kwenye Hansard na Msemaji wa Upinzani aliendela kutoa maoni yake.

## Mwongozo wa Spika

Mhe. George Mkuchika aliomba mwongozo kuhusu ukurasa wa 11 aya 6 ya Kambi ya Upinzani kuongelea mwenendo wa CDF – Mhe. Paresso alitaka kiache hotuba yao isomwe Waziri atapata muda wa kujibu – kiti kilitoa mwongozo aya ya 6 ukurasa wa 11 kuondolewa kwenye Hansard na Msemaji aliendelea kusoma hotuba yake kama alivyoelekezwa na kiti.

Mwongozo wa Spika

Mhe. George Mkuchika aliomba Mwongozo kwamba ukurasa 14 wa taarifa ya Upinzani inaongelea mwenendo wa Rais anapoongelea Rais kuamrisha wasiolipa umeme wakatiwe kinyume cha Kanuni ya 64.

Mhe. Matiko alisisitiza kwamba jambo hili alilisema na lilionekana kwenye television na siyo maneno ya Kambi. Kiti kilitoa mwongozo

maneno hayo yaondolewe kwenye Hansard na Msemaji aliendelea kutoa hotuba yake.

Mwongozo wa Spika

Mhe. Pendo Pendeza aliomba mwongozo kuhusu maneno ya retention allowance yaliyoko ukurasa wa 12 ambayo yameondolewa wakati maneno hayo yapo ukurasa wa 19 na hayajaondolewa – kiti kilitoa mwongozo kwamba yaliyoondolewa ni classified information.

Uchangiaji wa jumla ulifuata kwa wafuatao walipata nafasi ya kuchangia:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Fakharia Khamis | - | CCM |
| 2. | Mhe. Johnson Rweikiza | - | CCM |
| 3. | Mhe. Masoud Salim | - | CUF |

## VII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 7:00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11:00 jioni.

## VIII. BUNGE KURUDIA

Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia, mjadala wa Hoja ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa uliendea kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. | Mhe. Rhoda Edward Kunchela | - | CHADEMA |
| 5. | Mhe. Sophia Edson Mwakagenda | - | CHADEMA |
| 6. | Mhe. Saada Salum Mkuya | - | CCM |
| 7. | Mhe. Matar Ali Salum | - | CCM |
| 8. | Mhe. Khadija Aboud | - | CCM |
| 9. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso | - | CUF |
| 10. | Mhe. Maryam Salum Msabaha | - | CHADEMA |
| 11. | Mhe. Esther Nicholaus Matiko | - | CHADEMA |
| 12. | Mhe. Deogratias Francis Ngalawa | - | CCM |
| 13. | Mhe. Vedasto Mathayo Manyinyi | - | CCM |
| 14. | Mhe. Mbaraka Kitwana Dau | - | CCM |
| 15. | Mhe. Mwantum Dau Haji | - | CCM |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16. | Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu | - | CCM |
| 17. | Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangalah | - | NW-(AMJJW) |
| 18. | Mhe. Dkt. Susan Alphonce Kolimba | - | NW (MNUAA) |
| 19. | Mhe. George Mcheche Masaju | - | AG |

## IX. KUHITIMISHA HOJA

Mtoa Hoja Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi alihitimisha Hoja kwa kutoa majibu ya Hoja mbalimbali zilizotokana na Michango ya Wabunge. Alitoa Hoja na kuungwa Mkono.

## X. KAMATI YA MATUMIZI

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi ili kupitisha mafungu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo ni fungu 57 (Wizara), fungu 38 (Ngome) na fungu 39 (JKT).

### FUNGU 57 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.

1. Mhe. Martha Moses Mlata
2. Mhe. Richard Philip Mbogo
3. Mhe. Masoud Abdallah Salim, alitoa Hoja ya kutoa shilingi na kuchangiwa na:-

    - Mhe. Esther Nicholaus Matiko
    - Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala
    - Mhe. Riziki Shahari Mngwali
    - Mhe. Mwita Mwikabe Waitara
    - Mhe. Mwigulu Lameck Mchemba
    - Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni
    - Mhe. Ashatu Kachamba Kijaji

4. Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba
5. Mhe. Mathayo Vedasto Manyinyi

6. Mhe. Mwita Mwikabe Waitara alitoa shilingi na Hoja hiyo kuchangiwa na:-
   - Mhe. Ally Saleh Ally

   - Kutokana na kuisha kwa muda, Bunge liliingia kwenye hatua ya Guillotine na kupitisha mafungu yote kwa ujumla.

   - Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya kazi ya Kamati na kutoa Hoja ya Kuomba Bunge lipitishe Bajeti yake, Hoja iliungwa mkono, Bunge lilihojiwa na kupitisha Bajeti.

   **MWONGOZO**

   Mhe. Jenista Mhagama aliomba mwongozo kwa Kanuni ya 68 (7) kuhusiana na Maneno ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwenye Hotuba yake kwamba Taarifa ina maneno mengi ya uongo kuhusu Jeshi la Wananchi kwa nini Msemaji huyo asifute maneno hayo au kiti kitoe mwongozo.

   - Kiti kilimtaka Mbunge afute maneno hayo au apewe siku 2 hadi Ijumaa tarehe 19.5.2017 aje kuthibitisha maneno haya.

   - Mbunge alifuta maneo yaliyosemwa kwenda kinyume.

## XI. KUAHIRISHA BUNGE

Bunge liliahirishwa saa 1: 50 usiku hadi kesho tarehe 17 Mei, 2017 saa 3:00 asubuhi.